# USHINDE ULIMWENGU na Upate Pumziko

**Na Rais Russell M. Nelson**
Rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

## Kwa sababu YESU KRISTO aliushinda huu ulimwengu

ulioanguka na kwa sababu Yeye aliteseka kwa ajili ya kila mmoja wetu, wewe pia unaweza kuushinda huu ulimwengu uliojaa dhambi, wenye ubinafsi na mara nyingi wenye kuchosha.



Kadiri unavyotubu kwa uhakika na kutafuta usaidizi Wake, unaweza kuinuka juu ya huu ulimwengu wenye hatari na kupata *pumziko* la kweli.

## NI KWA JINSI GANI TUNAUSHINDA ULIMWENGU?



Kutafuta na kufuata misukumo ya Roho.



Kutubu kila siku na kushika maagano ambayo hutupatia nguvu.



Baki katika njia ya agano.

## INAMAANISHA NINI KUUSHINDA ULIMWENGU?

Inamaanisha:

- Kushinda vishawishi vya kujali zaidi kuhusu mambo ya ulimwengu kuliko mambo ya Mungu.



- Kutumaini mafundisho ya Kristo zaidi kuliko falsafa za wanadamu.



- Kufurahia katika ukweli, kuukataa udanganyifu na kuwa "mfuasi mnyenyekevu wa Kristo."



- Kuchagua kujitoa kwenye kitu chochote kinachomuweka Roho mbali na kuwa tayari "kuachia" hata dhambi tuzipendazo.



- Kukua zaidi katika kumpenda Mungu na Mwanae Mpendwa kuliko kumpenda mtu mwingine yeyote au kitu chochote.





**MWOKOZI *HUTUINUA* SISI** juu ya mvutano wa ulimwengu huu ulioanguka kwa kutubarika na hisani zaidi, unyenyekevu zaidi, ukarimu zaidi, wema zaidi, nidhamu binafsi, amani na *pumziko*.

**KWA SABABU YESU KRISTO ALIUSHINDA ULIMWENGU HUU, NAWE PIA UNAWEZA.**

*Kutoka kwenye hotuba ya mkutano mkuu wa Oktoba 2022.*

VIELELEZO NA BRYAN BEACH